# 16- Utekelezaji Wa Hajj

## Tarehe 8 Dhul-Hijjah Siku ya *At-Tarwiyah*

- Tarehe 8 Dhul-Hijjah inajulikana kuwa ni siku ya *At-Tarwiyah* ambayo Mahujaji wataelekea *Minaa*. Ikiwa ni mwenye kutekeleza *Hajj Tamattu'*, unatakiwa siku hiyo kujitwaharisha tena kuingia katika Ihraam kama ulivyofanya wakati wa 'Umrah mahali hapo ulipo hotelini. Utavaa Ihraam yako na kusema:

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ حَجًّا

***Labbayka-Allaahumma Hajjaa***

لَبَّيْكَ حَجّاً لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ، لا شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ، إنَّ الْحَمْدَ، وَالنِّعْمَة، لَكَ وَالْمُلْكُ، لا شَرِيكَ لَكَ

***Labbayka Hajja labbayka-Allaahumma labbayk, labbayka, laa shariyka Laka labbayk, Innal-Hamda, wan-ni'matah Laka wal-Mulk, laa shariyka Lak***

- Ikiwa utakhofu kuwa jambo litakuzuia kukamilisha Hajj yako basi useme:

وَإِنْ حَبَسَنِي حَابِسٍ فَمَحَلِّي حَيْثُ حَبَسْتَنِي

**((*Ikiwa nitazuiliwa na kizuizi chochote sehemu yangu ni popote nilipozuiliwa*)).**

- Ikiwa huna khofu kama hiyo basi hakuna haja ya kujishurutisha hivyo.

- Kisha utakwenda *Minaa* na huko utaswali Swalaah ya Adhuhuri, Alasiri, Magharibi, 'Ishaa na Alfajiri. Utaswali *qaswran* Swalaah za rakaa nne kuwa mbili mbili kila moja bila ya *jam'an*, yaani kuswali kila

*Swalaah* kwa wakati wake ila uzifupishe tu kama alivyofanya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

## Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa

- Kutokuleta *Talbiyah* - wengi hawafanyi hivo wakighafilika nayo jambo ambalo ni kinyume na Sunnah kwani *Talbiyah* inamalizika baada ya *Jamrat Al-'Aqabah*.

- Kujumuisha Swalaah badala ya kufupisha pekee. Ni kinyume na Sunnah kuunga Swalaah za Adhuhuri na Alasiri, na pia Magharibi na 'Ishaa. Inavyopasa ni kuziswali kila moja kwa wakati wake huku ukizifupisha.

- Mahujaji kupoteza muda wao katika mahema kwa kupiga soga badala ya kufanya *dhikru-Allaah* au badala ya kuelimishana hapo mambo ya Dini na hasa yanayohusu utekelezaji sahihi wa 'ibaadah hii ya fardhi. Mahujaji wengi kabisa wanafika huko kutekeleza fardhi hii wakiwa hawana elimu ya kutosha ya jinsi ya kuitekeleza 'ibaadah hii, na hapo ni fursa ya kuwaelimisha badala ya kupoteza muda kwa mambo yasiyofaa.

- Kukusanyika kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwa pamoja, kuomba du'aa kwa pamoja, kusoma Mawlid, na kusoma adhkaar zisizokuwa zenye dalili na 'ibaadah nyinginezo zisizothibiti katika Sunnah ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

## Tarehe 9 Dhul-Hijjah – Siku Ya *'Arafah*

Hatua za kufanya:

- Jua litakapochomoza siku ya pili ambayo ni tarehe 9 Dhul-Hijjah, utakwenda *'Arafah* na huko utaswali Adhuhuri na Alasiri *jam-'an* wa *qaswran* wakati wa Adhuhuri. Kisha utabakia katika Msikiti wa Namirah au maeneo yoyote ya *'Arafah* pale mtakapowekwa

mpaka jua litakapokuchwa. Hapo kaa kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kila aina ya kumdhukuru; kusoma Qur-aan, *istighfaar, tasbiyh, tahmiyd, tahliyl, takbiyr,* kuomba du'aa kwa wingi uwezavyo huku ukielekea Qiblah na sio kuelekea jabali la '*Arafah*.

Usipojaaliwa kuweko katika Msikiti wa Namirah karibu na jabali la '*Arafah* basi popote utakapokuwa kwani Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alisimama katika jabali la '*Arafah* na akasema:

((وَوَقَفْتُ هَاهُنَا وَعَرَفَةُ كُلُّهَا مَوْقِفٌ))

***((Nimesimama hapa na 'Arafah yote ni kisimamo [cha 'Arafah])).*[1]**

Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa akiomba:

**لا إِلَهَ إلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ ولَهُ الحَمْدُ وهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ**

***Laa Ilaaha Illa-Allaah Wahdahu laa shariyka Lah, Lahul-Mulku walahul-Hamud wa-Huwa 'alaa kulli shay-in Qadiyr***

"Hapana ilaah (muabudiwa wa haki) ila Allaah, Hana mshirika, ni Wake Ufalme na ni Zake Sifa njema zote, Naye juu ya kila kitu ni Muweza". [2]

- Utakapochoka unaruhusiwa kuzungumza na wenzako kidogo mas-alah ya Dini, au kusoma vitabu vyenye faida khasa kuhusu ukarimu, Rahmah ya Allaah (سبحانه وتعالى), neema Zake kwetu ili uzidi kupata matumaini kutoka kwa Allaah (سبحانه وتعالى) ya kufutiwa dhambi na kutakabaliwa unayoyahitaji. Kisha endelea kuomba du'aa na kuhakikisha kuwa unatumia wakati wako wa mwisho wa siku hiyo katika du'aa nyingi kwa sababu du'aa zilizo bora kabisa ni *du'aa* za siku ya '*Arafah*.

[1] Muslim.

[2] At-Tirmidhiy na ameisahihisha Al-Abaaniy katika *Swahiyh At-Tirmidhiy* 3585.

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa *'Arafah***

- Baadhi ya Mahujaji wanapiga kambi nje ya maeneo ya *'Arafah* na kubakia hapo hadi jua kuzama, kisha wanaelekea *Muzdalifah* bila ya kusimama *'Arafah* kama inavyopasa. Hili ni kosa kubwa ambalo linabatilisha Hijja yao kwani kusimama *'Arafah* ni kilele cha Hajj na pia ni fardhi kubakia ndani ya eneo la *'Arafah* na si nje ya eneo lake. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

  **((الْحَجُّ عَرَفَة، مَنْ جَاءَ قَبْلَ طُلُوعِ الْفَجْرِ مِنْ لَيْلَةِ جَمْعٍ فَقَدْ أَدْرَكَ الْحَجّ))**

  ***((Al-Hajj ni 'Arafah, atakayekuja kabla kutoka Alfajiri usiku wa kujumuika atakuwa ameipata Hajj))***.[3]

- Kuondoka *'Arafah* kabla ya jua kuzama hairuhusiwi kwa sababu Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alibakia *'Arafah* hadi jua kuzama kabisa.

- Kujilazimisha katika zahma ya watu kupanda jabali la *'Arafah* hairuhusiwi, kwa sababu inakusababisha madhara na madhara kwa Mahujaji wengine. Eneo lote la *'Arafah* linahesabiwa kuwa ni kisimamo cha *'Arafah*, na si kupanda jabali la *'Arafah* wala kuswali katika hilo jabali au karibu yake hata idhaniwe kuwa mtu amepata kisimamo cha *'Arafah*.

- Kuomba du'aa akiwa anaelelekea jabali la *'Arafah* ni makosa kwa sababu inapasa kuelekea Qiblah wakati wa kuomba du'aa.

- Kurundika chungu ya mchanga au vijiwe siku ya *'Arafah* katika sehemu fulani, jambo ambalo haliko katika shariy'ah ya Allaah.

- Kulipa jina Jabali la *'Arafah* kuwa ni *Jabal Ar-Rahmah*.

---

[3] *Swahiyh Al-Jaami'*.

***Muzdalifah***

- Jua litakapozama utaondoka *'Arafah* kwenda *Muzdalifah* na huko utaswali Magharibi na 'Ishaa. Ikiwa utachoka au umepungukiwa na maji, unaruhusiwa kuunganisha Magharibi na 'Ishaa. Ikiwa utakhofu kuwa hutofika *Muzdalifah* mpaka baada ya usiku wa manane, basi swali kabla ya kufika huko kwani hairuhusiwi kuchelewesha Swalaah mpaka usiku wa manane.

- Utabakia huko *Muzdalifah* usiku kukesha, na hapo omba sana du'aa na mdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) mpaka Alfajiri. Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ فَإِذَآ أَفَضۡتُم مِّنۡ عَرَفَٰتٖ فَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ عِندَ ٱلۡمَشۡعَرِ ٱلۡحَرَامِۖ وَٱذۡكُرُوهُ كَمَا هَدَىٰكُمۡ وَإِن كُنتُم مِّن قَبۡلِهِۦ لَمِنَ ٱلضَّآلِّينَ ١٩٨ ثُمَّ أَفِيضُواْ مِنۡ حَيۡثُ أَفَاضَ ٱلنَّاسُ وَٱسۡتَغۡفِرُواْ ٱللَّهَۚ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٞ رَّحِيمٞ ١٩٩ ﴾

**((Basi mtakapomiminika kutoka *'Arafaat* mdhukuruni Allaah kwenye *Mash'aril- Haraam* (Muzdalifah) na mdhukuruni Yeye kama Alivyokuongozeni kwani hakika mlikuwa kabla ya hapo miongoni mwa waliopotea. Kisha miminikeni kutoka pale wamiminikapo watu; na ombeni maghfirah kwa Allaah. Hakika Allaah ni *Ghafuwrur-Rahiym* (Mwenye kughufuria - Mwenye kurehemu))).[4]**

- Utaswali Alfajiri mapema kwa adhaan na Iqaamah, kisha utaelekea *Mash'aril-Haraam* na utafanya *tahliyl*, yaani utasema ***"Laa Ilaaha Illa***

[4] Suratul Baqarah (2: 198).

***Allaah***" pia "***Allaahu Akbar***" na utaomba du'aa mpaka kupambazuke vizuri. Ikiwa hukujaaliwa kwenda *Mash'aril-Haraam*, utaomba hapo hapo ulipo kutokana na kauli ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

((وَوَقَفْتُ هَاهُنَا وَجَمْعٌ كُلُّهَا مَوْقِفٌ))

***((Nimesimama hapa na kote hapa ni kisimamo [cha Muzdalifah*]***))***.[5]

Unapoomba du'aa uelekee Qiblah na huku ukinyanyua mikono.

- Utaondoka *Muzdalifah* kuelekea *Minaa* huko utaokota vijiwe kwa ajili ya kurusha katika *Jamrat Al-'Aqabah*.

## Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa *Muzdalifah*

- Kutokumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) usiku huo na badala yake kulala tu na hali hapo ni mahali patukufu mno na panapotakiwa kumdhukuru mno Allaah (سبحانه وتعالى) kama ilivyotajwa katika Aayah hapo juu.

- Baadhi ya Mahujaji wanapofika tu *Muzdalifah* na kabla ya kuswali Swalaah za Magharibi na 'Ishaa huanza kukusanya vijiwe vya kurusha katika *Jamaraat*.

- Kudhania kwamba vijiwe lazima viokotwe *Muzdalifah* na hali vinaweza kuokotwa popote katika maeneo ya Al-Haram ikiwa ni *Muzdalifah* au *Minaa*. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) hakuamrisha vijiwe vya *Jamrat Al-'Aqabah* viokotwe *Muzdalifah* bali Maswahaba walimuokotea yeye vijiwe asubuhi baada ya kuondoka *Muzdalifah* na kuingia *Minaa*. Aliokotewa vijiwe vyote viilobakia kutoka *Minaa* pia.

## *Minaa – Ar-Ram-y* Katika *Jamaraat*

---

[5] Muslim.

Ukiwa ni dhaifu na huwezi kustahamili zahma za watu wakati wa *Ar-Ram-yu*, (kama mwanamke na mtu mzima), basi unaruhusiwa kwenda *Minaa* mwisho wa usiku huo kurusha vijiwe katika *Jamrat Al-'Aqabah* pekee kabla ya zahma ya watu kuwa kubwa.

Kurusha vijiwe kuna maana zifuatazo:

**i-** Imekusudiwa kuwa ni njia ya kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwa hiyo ni kitendo cha 'ibaadah.

**ii-** Kufuata mafunzo ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) aliposema: *((Chukueni kwangu taratibu zenu [za Hajj])).*

**iii-** Kukumbuka kisa cha Nabiy Ibraahiym na mwanawe Nabiy Ismaa'iyl (عليهما السلام).

**iv-** Kumhizi shaytwaan atakapoona ummah wa watu wanarusha vijiwe mahali alipomtia shaka na kutaka kumpotosha Nabiy Ibraahiym (عليه السلام).

**Tarehe 10 Dhul-Hijjah**

Siku hii ni siku iliyo bora kabisa kwa Allaah (سبحانه وتعالى) kama alivyosema Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

**((إِنَّ أَعْظَمَ اْلأَيَّامِ عِنْدَ الله تبارك وتعالى يَوْمُ النَّحْرِ ثُمَّ يَوْمُ الْقَرِّ))** رواه أبو داود والنسائي وصححه الألباني

***((Siku iliyo tukufu kabisa kwa Allaah ni siku ya kuchinja, kisha siku ya kutulia)).***[6] (yaani siku ya kukaa *Minaa*)

Karibu na jua kuchomoza utaondoka *Muzdalifah* kuelekea *Minaa*. Unapokwenda unatakiwa uendelee kuleta *Talbiyah* mpaka umalize

[6] Abu Daawuwd na An-Nasaaiy na ameisahihisha Al-Abaaniy.

kurusha vijiwe katika *Jamrah* hiyo ya *Al-'Aqabah* ndipo *Talbiyah* inamalizika. Utakapofika utafanya yafuatayo:

- Utarusha vijiwe saba kimoja baada ya kimoja katika Al-Jamrat Al-'Aqabah (*Jamratul-Kubraa*) pekee ambalo liko karibu na mnara wa Makkah na kusema ifuatavyo kwa kila kijiwe utakachokirusha:

**اللهُ أَكْبَرَ**

***Allaahu Akbar***

- Utachinja mnyama, na kula baadhi ya nyama na utatoa nyingine kuwapa masikini. Kuchinja ni fardhi kwa wale wanaofanya Hajj ya *Tamattu'*u na *Qiraan*. (Kwa hali ilivyo sasa huwa haiwezekani kufanya hivi, hivyo unaweza kutekeleza kama unavyoamrishwa yaani kulipa na kuacha jukumu hili kwa serikali ifanye kazi ya kuchinja).

- Utanyoa au kukata nywele. Inapendekezwa kunyoa kuliko kukata kama alivyosema Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).[7] Mwanamke atakata nywele zake urefu wa ncha ya kidole.

- Utakwenda Makkah kufanya *Twawaaful-Ifaadhwah* na *As-Sa'-y*. Ni Sunnah kujitia manukato kabla ya kwenda Makkah (kwa wanaume) kutokana na kauli ya Mama wa Waumini 'Aaishah (رضي الله عنها) kwamba:

**كُنْتُ أُطَيِّبُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لإِحْرَامِهِ حِينَ يُحْرِمُ وَلِحِلِّهِ قَبْلَ أَنْ يَطُوفَ بِالْبَيْتِ**

"Nilikuwa nikimpaka manukato Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) kabla ya kuingia katika Ihraam na baada ya kutoka katika Ihraam kabla ya kutufu *Al-Ka'bah.*"[8]

Mambo manne hayo yafanywe kama ilivyo taratibu yake ikiwezekana, lakini hakuna ubaya au sharti ikiwa mtu atatanguliza kitendo chochote kabla ya chengine.

---

[7] Tazama 'Utekelezaji wa 'Umrah' baada ya As-Sa'-y.
[8] Al-Bukhaariy na Muslim.

- Imeruhusika kuchelewesha *Twawaaful-Ifaadhwah* na *As-Sa'-y* kwa aliye na dharura kurudi Makkah, na inaweza ikacheleweshwa mpaka tarehe 12. Utakapomaliza hayo mambo matatu utaruhusika kujitoa katika Ihraam ndogo. Na unaweza kuvaa nguo zako za kawaida na kufanya kila jambo la halali isipokuwa kuingia katika kitendo cha ndoa, huku ukisubiri kumaliza *Twawaaful-Ifaadhwah* na *As-Sa'-y,* na hapo utakapomaliza ndipo utaruhusika kujivua kabisa Ihraam yako na kuwa huru na yote yaliyoharamishwa wakati wa Ihraam.

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa Katika *Jamaraat***

- Baadhi ya Mahujaji wanadhania kwamba kurusha vijiwe katika nguzo za *Jamaraat* ni kumpiga shaytwaan, hivyo wanapinduka mipaka katika kitendo hiki cha 'ibaadah.

- Wengine wanarusha vijiwe vikubwa, viatu, mbao n.k. na hurusha kwa ghadhabu. Wengine hufikia hadi kutukana! Hivyo ni kusababisha madhara kwa Mahujaji wengine kwani mtu anaweza kurusha jiwe kubwa kwa mbali likampiga Haaj aliye mbele yake badala ya kupiga nguzo. Vijiwe vidogo vyenye ukubwa wa harage au kunde au punje za mahindi ndio bora zaidi kuvitumia.




- Kuacha kwao kuomba du'aa baada ya kutupa vijiwe mnara wa kwanza na wa pili katika yale masiku yanayoitwa *Ayyaam At-Tashriyq*. Ilivyothibiti ni kuwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa pindi akimaliza kurusha vijiwe minara miwili likuwa akisimama na akielekea Qiblah na kunyanyua mikono yake na kuomba du'aa ndefu. Na miongoni mwa sababu za watu kuacha kufanya hivi aidha kwa kutokujua au kupupia kwao kutaka kumaliza haraka kurusha vijiwe waondoke.

- Kusababisha zahma, kusukumana na kugombana na wengine katika maeneo hayo. Inavyopasa ni kuwa na upole na kurusha vijiwe bila ya madhara kwa wengine.

- Kurusha vijiwe vyote kwa mara moja. 'Wanachuoni wamesema kwamba hii itahesabika kuwa ni kama kurusha kijiwe kimoja kwa

sababu shariy'ah imetaja kurusha kijiwe kimoja baada ya kimoja na huku Haaj anasema 'Allaahu Akbar' kila kijiwe kimoja kinaporushwa.

- Kumuwakilisha mtu kurusha vijiwe, kwa kukhofia zahma au tabu na mashaka, na hali Haaj mwenyewe anao uwezo wa kutekeleza 'ibaadah hii. Wagonjwa tu na wale walio dhaifu ndio wanaruhusiwa kuwakilishwa na mtu kufanya 'amali hii. Ama kila mwenye uwezo na afya njema akarushe vijiwe mwenyewe pasina kuwakilishwa na Mtu. Watu wafahamu kuwa Hija ni moja kati ya aina za jihaad ambayo ni lazima mwenye kuhiji akabiliane na tabu mbalimbali na lazima aikamilishe 'ibaadah hii kama alivyoamrisha Allaah na Rasuli Wake.

- Kuzidisha kwao du'aa wakati wa kurusha vijiwe, yaani du'aa ambazo hazikuthibiti katika Sunnah kama kusema kwao; "Ee Allaah! Jaalia vijiwe hivi kuwa ni radhi Kwako na ni ghadhabu kwa shaytwaan". Mara nyingine wao huacha Takbiyrah iliyothibiti kutoka kwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

- Baadhi ya Mahujaji huosha vijiwe jambo ambalo halimo katika mafunzo ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

**Tarehe 11, 12 na 13 Dhul-Hijjah**

Kubakia *Minaa* masiku haya kumaliza kurusha vijiwe katika Jamrah zote tatu kuanzia *Jamrat Asw-Swughraa, Jamrat Al-Wuswtwaa* na *Jamrat Al-'Kubraa*. Na hizi ni siku tulizoamrishwa kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwa wingi:

﴿ ۞ وَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ فِيٓ أَيَّامٖ مَّعۡدُودَٰتٖۚ فَمَن تَعَجَّلَ فِي يَوۡمَيۡنِ فَلَآ إِثۡمَ عَلَيۡهِ وَمَن تَأَخَّرَ فَلَآ إِثۡمَ عَلَيۡهِۖ لِمَنِ ٱتَّقَىٰۗ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَٱعۡلَمُوٓاْ أَنَّكُمۡ إِلَيۡهِ تُحۡشَرُونَ ٢٠٣ ﴾

**((Na mdhukuruni Allaah katika siku za kuhesabika. Atakayeharakisha (kuondokwa kwake) katika siku mbili, basi hakuna dhambi juu yake; na atakayechelewesha (mpaka siku ya**

**tatu) basi hakuna dhambi juu yake; kwa mwenye kuwa na taqwa. Na mcheni Allaah na jueni kwamba Kwake mtakusanywa.))**[9]

Baada ya kufanya *Twawaaf* na *As-Sa'-y* utarudi *Minaa* kulala huko usiku wa tarehe 11 na 12 Dhul-Hijjah.

- Utarusha vijiwe Jamrah zote tatu jioni siku ya tarehe 11 na 12 Dhul-Hijjah. Utaanza kwanza *Jamrat Asw-Swughraa* ambayo iko mbali na Makkah, kisha utaelekea Qiblah na kuomba du'aa ndefu kwa kunyanyua mikono. Kisha utarusha *Jamrat Al-Wuswtwaa*, kisha utaelekea Qiblah na kuomba du'aa ndefu na kunyanyua mikono. Kisha *Jamrat Al-Kubraa* (*Jamrat Al-'Aqabah*) lakini ukimaliza hapo huombi du'aa bali utaondoka. Katika kila Jamrah utarusha vijiwe saba, moja baada ya moja na huku ukisema '***Allaahu Akbar'*** kwa kila kijiwe unachorusha.

- Haipasi kuacha kuomba du'aa tena iwe ndefu ikiwezekana baada ya kurusha vijiwe katika *Jamrat Asw-Swughraa* na *Jamrat Al-Wuswtwaa* kwani ni Sunnah na watu wengi sana hawatekelezi hivi aidha kwa kutokujua au kupuuza. Na kila inapokuwa Sunnah haitekelezwi ndipo inapokuwa haitambuliki kwa watu na huenda ikaachwa kabisa na kupotea.

| **Tarehe** | ***Jamrat Asw-Swughraa*** | **Du'aa** | ***Jamrat Al-Wustwaa*** | **Du'aa** | ***Jamrat Al-Kubraa*** <br> ***(Jamrat Al-'Aqabah)*** | **Du'aa** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **10** | **X** | **X** | **X** | **X** | √ | **x** |
| **11, 12, 13** | √ | √ | √ | √ | √ | **X** |

[9] Al-Baqarah (2: 203).

- Hairuhusiwi kurusha vijiwe kabla ya Adhuhuri katika siku mbili hizi.

- Ni bora kabisa kutembea kwenda kurusha vijiwe, ingawa kipando kinaruhusiwa.

- Ikiwa una haraka ya kurudi, baada ya kurusha vijiwe siku ya 12 Dhul-Hijjah, unaweza kuondoka *Minaa* lakini iwe kabla ya jua kuzama. Lakini ukipenda kuzidisha makazi yake, ambayo ni bora zaidi, basi ulale *Minaa* usiku wa 13 na kuendelea kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) na kurusha vijiwe *Jamaraat* jioni kama ulivyofanya siku ya kumi na mbili. Dalili na kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى) iliyotajwa juu.

## Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa *Ayyaam At-Tashriyq*

- Baadhi ya Mahujaji hawalali siku ya tarehe 11 na 12 bali wanakuwa nje ya *Minaa* bila ya udhuru.

- Wengineo huondoka mchana na kwenda Makkah kukimbia kubakia katika mahema huko *Minaa*.

- Wengine huchanganya katika kurusha vijiwe na kuanza ndivyo sivyo katika *Jamaraat*. Tazama chati juu.

## *Twawaaf Al-Wadaa'i*

- Utakapokuwa tayari kusafiri, kabla ya kuondoka fanya *Twawaaf Al-Wadaa'i* ambayo ni mizunguko saba katika *Al-Ka'bah* kutokana na kauli ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

**((لَا يَنْفِرَنَّ أَحَدٌ حَتَّى يَكُونَ آخِرُ عَهْدِهِ بِالْبَيْتِ))**

***((Asikimbie mtu [asiondoke zake] mpaka iwe shughuli yake [kitendo chake cha mwisho] katika Nyumba [Al-Ka'bah*]*))*.[10]

- Wanawake wenye hedhi na nifaas hawana lazima kufanya *Twawaaf Al-Wadaa'i* kutokana na dalili ifuatayo:

أُمِرَ النَّاسُ أَنْ يَكُونَ آخِرُ عَهْدِهِمْ بِالْبَيْتِ إِلَّا أَنَّهُ خُفِّفَ عَنْ الْحَائِضِ

"Aliamrisha watu iwe shughuli zao za mwisho ni *Al-Ka'bah* isipokuwa waliruhusiwa (wanawake) wenye hedhi."[11]

- Ikiwa baada ya *Twawaaf Al-Wadaa'i* umebakia kidogo wakati huo unasubiri wenzako au kipando chako au kununua kitu njiani hakuna ubaya, wala hakuna haja ya kurudia *Twawaaf Al-Wadaa'i* isipokuwa ikiwa umetia niyyah ya kuchelewesha safari yako; mfano ukitaka kuondoka mwanzo wa siku, ukatufu *Al-Ka'bah*, kisha ukachelewesha safari hadi mwisho wa siku, basi itakulazimu urudie kutufu *Al-Ka'bah* ili iwe ni kitendo chako cha mwisho.

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa Kuhusu *Twawaaf Al-Wadaa'i***

- Kuondoka *Minaa* wakaenda Makkah na wakafanya *Twawaaf Al-Wadaa'i* kisha wakarudi tena *Minaa* kumalizia kurusha vijiwe ndipo baadaye waondoke Makkah. Kufanya hivyo, ina maana kwamba, kurusha vijiwe ni kitendo cha mwisho kufanya kabla ya kuondoka Makkah na hii ni kinyume na alivyoagiza Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

- Kukaa kwao kitambo Makkah baada ya kutufu *Twawaaf Al-Wadaa'i* na hivyo ifahamike kuwa jambo lao la mwisho walilofanya si kutufu.

---

[10] Muslim.
[11] Al-Bukhaariy na Muslim.

Na hili pia ni kinyume na amri ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kwani Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) Alifanya *Twawaaf Al-Wadaa'i* kisha akaondoka na hivi ndivyo walivyokuwa wakifanya Maswahaba zake. Isipokuwa Wanachuoni wameruhusu mtu kubakia kidogo baada ya kuiaga *Al-Ka'bah* kama kuna dharura kubwa kama ya kuingia wakati wa Swalaah au kuswalia jeneza au jambo lenye kuambatana na safari yake kama kununua kitu au kusubiri kidogo wenzake. Ama yule ambae atakaa Makkah baada ya *Twawaaf Al-Wadaa'i* pasina dharura atalazimika airudie *Twawaaf* baadaye.

- Kutoka katika milango ya *Al-Ka'bah* hali ya kuwa wanapiga piga vichogo vyao wakidhani kuwa kwa kufanya hivyo wanaitukuza *Al-Ka'bah* kumbe wanazua katika Dini na hivyo kumaliza 'ibaadah hii tukufu kwa kufanya bid'ah.

- Kuilekea kwao *Al-Ka'bah* wakiwa mlangoni wamemaliza kutufu *Twawaaf Al-Wadaa'i* na wakawa wanaomba du'aa zao kama wenye kuiaga *Al-Ka'bah*. Na jambo hili halikuthibiti kutoka kwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).